# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Tatu



Taasisi ya Elimu Tanzania

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Uraia na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Tatu



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 563

Jina la Chapisho: Uraia na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-315-1

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Julai, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Tatu katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2015.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza 2018
Toleo la Pili 2021

ISBN 978 - 9987 - 09- 315 - 1

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255735041170/+255735041168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE USE ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kupiga chapa, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Shukurani**.................................................................... v

**Utangulizi**.................................................................... vi

**Sura ya Kwanza**

Tuipende na kuiheshimu jamii yetu ........................................ 1

**Sura ya Pili**

Tuipende shule yetu.................................................................. 9

**Sura ya Tatu**

Tuipende nchi yetu................................................................. 16

**Sura ya Nne**

Tuithamini jamii yetu.............................................................. 25

**Sura ya Tano**

Tuwajibike............................................................................. 41

**Sura ya Sita**

Tuwe wastahimilivu ................................................................ 52

**Sura ya Saba**

Tuwe waadilifu....................................................................... 60

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Nane**

Tudumishe amani.................................................... 69

**Jaribio la kwanza** ................................................ 85

**Jaribio la pili** .................................................... 88

**Nyimbo za noti** ................................................... 91

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi na maandalizi ya kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui na uhariri wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa ukaribu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.



**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na Muhtasari wa Uraia na Maadili wa Mwaka 2016 ambao unazingatia ujenzi wa umahiri.

Muundo wa kitabu hiki umegawanyika katika sura kuu nane ambazo nazo zinaundwa na sura ndogondogo. Katika kila sura kuna maswali, mazoezi, kazi za kufanya kwa ajili ya mwanafunzi kujenga umahiri unaokusudiwa kujengwa katika sura husika. Ufafanuzi wa maneno mapya na magumu umetolewa mwishoni mwa kila sura.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

# Tuipende na kuiheshimu jamii yetu

Jamii ni watu wanaoishi pamoja na kushirikiana katika shughuli mbalimbali. Wanajamii wema hutengeneza jamii bora. Katika sura hii utajifunza jinsi ya kuishi vizuri na wanajamii wengine. Ili kuishi vizuri na wanajamii wengine unapaswa kujipenda, kujitambua na kuwapenda wengine.

## Kujipenda na kuwapenda wengine

### Kujipenda

Kujipenda ni kujithamini na kujikubali. Mtoto anayejipenda anatunza afya yake. Vilevile, anaepuka matendo mabaya na anakuwa na tabia njema wakati wote.

Angalia picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**



**B.**



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

C.



D.



**Kielelezo namba 1** Matendo ya kujipenda

## Maswali

1. Picha hizi zinaonesha matendo gani?
2. Taja matendo ya kujipenda unayoyafahamu.
3. Je, ni matendo gani ya mtu asiyejipenda unayoyafahamu?

## Kazi ya kufanya

Andika kwenye daftari lako matendo matatu ya kujipenda unayoyatenda katika kila eneo.

(a) nyumbani
(b) shuleni
(c) kwa majirani wanaokuzunguka

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

1. Taja matendo matano ya kujipenda unayoyafahamu.
2. Taja matendo matano yanayofanywa na mtu asiyejipenda.
3. Faida za usafi wa mwili na mavazi ni __________, __________ na __________ .
4. Soma matendo yafuatayo, kisha eleza matendo haya yanatufundisha nini?
   (a) Mwanafunzi anapiga mswaki na kuoga kila siku.
   (b) Mwanafunzi ana marafiki wenye tabia njema.
   (c) Mwanafunzi amevaa nguo safi na nadhifu.

## Kuwapenda wengine

Matendo kama kusalimiana kwa lugha inayofaa na kuwasikiliza wengine yanaashiria kuishi vizuri. Vilevile, kuwasaidia na kuwaelekeza vizuri wengine inaonesha kuwa una upendo. Mwanafunzi anayewapenda watu wengine huwa tayari kuwasiliana nao na kuwasaidia.Hebu jiulize, utachukua hatua gani ikiwa,

(a) mwanafunzi mwenzako amejikwaa na kuanguka.
(b) mdogo wako analia.
(c) mtu asiyeona yuko kandokando ya barabara akihitaji kuvuka.
(d) mwanafunzi mwenzako hana kalamu wakati wewe una kalamu mbili.
(e) mwalimu anaingia darasani kwenu.
(f) umeamka asubuhi na kukutana na watu wakubwa kwako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mwanafunzi anayewapenda wengine huwatakia heri na huwapa pole wanapopata matatizo. Vilevile, huwashukuru wanapomsaidia na huomba msamaha anapowakosea.

### Maswali

1. Ni matendo gani ya upendo unayoyafahamu?
2. Je, ni matendo gani ya upendo unayoyafanya kwa wengine ukiwa nyumbani?
3. Je, ni matendo gani ya upendo wanakufanyia wenzako mnapokuwa shuleni?
4. Je, utawasaidiaje wenzako kutenda matendo ya upendo?

FOR ONLINE USE ONLY

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Nuru na Elifuraha ni marafiki. Wote wawili wanasoma darasa la tatu katika Shule ya Msingi Tupendane. Marafiki hawa mara nyingi hutembeleana nyumbani. Siku moja Nuru aliamua kumtembelea Elifuraha nyumbani kwao. Alimkuta mama yake Elifuraha amepumzika barazani. Siku hiyo Elifuraha hakuwepo nyumbani. Alimsogelea na kumwamkia mama yake Elifuraha.

Mama yake Elifuraha alimweleza Nuru kuwa anaumwa sana. Nuru alimpa pole na muda huohuo alikwenda kutafuta msaada kwa majirani. Majirani wawili walifika na kumpeleka mgonjwa hospitalini. Alipofika hospitalini alipatiwa matibabu na kuruhusiwa kurudi nyumbani. Elifuraha aliporudi nyumbani alimshukuru Nuru kwa upendo aliouonesha kwa mama yake.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Je, habari uliyoisoma inatufundisha nini?
2. Je, ni matendo gani ya kuwapenda watu wengine yaliyopo katika habari hii?
3. Je, ni matendo gani mengine ya kuwapenda watu wengine unayoyafahamu?
4. Ingekuwa ni wewe ungemsaidiaje mama Elifuraha tofauti na Nuru alivyofanya?

**Kazi ya kufanya**

Andika hatua utakazochukua kumsaidia mwanafunzi mwenzako aliyeumia mguu wakati akicheza mpira shuleni.

## Kujitambua

Kujitambua ni hali ya kujua uwezo wako wa kutenda mambo.Yapo mambo unayoweza kutenda vizuri na yapo usiyoweza kutenda. Uwezo wa kutenda jambo jema kwa ustadi unaitwa kipaji.

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**



**B.**



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

C.



D.



E.



**Kielelezo namba 2** Matendo yanayoonesha vipaji

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Je, ni matendo gani unayoyaona kwenye picha hizi?
2. Wewe unapendelea tendo lipi zaidi?
3. Ni matendo gani kwenye picha marafiki zako watayatenda kwa ustadi zaidi?
4. Wewe una vipaji gani?
5. Ni vipaji gani vingine walivyonavyo marafiki zako?
6. Kati ya matendo yafuatayo ni yapi yanayoonesha vipaji? Pigia mstari majibu yako.
   (a) Kuimba, kucheza ngoma, kulia, kulala, kuhuzunika
   (b) Kuchora, kukaa, kufuma, kukimbia na kupiga makofi
   (c) Kupiga kelele, kupaka rangi, kuigiza na kucheza mpira.

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Mwalimu Dina anafundisha Uraia na Maadili katika Shule ya Msingi Misufini. Siku moja aliwataka wanafunzi wa darasa la tatu kueleza vipaji walivyonavyo. Kila mwanafunzi alipewa nafasi ya kujieleza. Ashura na Juma walisema wanaweza kuchora vizuri sana. Mwalimu aligundua Ashura na Juma ni hodari wa kuchora. Sara na Musa walijitokeza na kusema wanaweza kuimba vizuri sana. Grace na Zuberi walisema kwamba wao wanaweza kucheza mpira wa miguu kwa ustadi. Hii ilimfanya mwalimu Dina abaini kuwa wanafunzi wake walikuwa na vipaji tofauti tofauti. Baada ya hapo, Mwalimu Dina aliweka mipango ya kukuza vipaji vya wanafunzi. Aliwasihi kila mmoja aongeze bidii katika kukuza kipaji alichonacho.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Maswali

1. Ni vipaji gani vinavyotajwa katika habari hii?
2. Je, wewe una kipaji gani?
3. Je, utafanya nini kukuza kipaji chako?

### Zoezi la 2

1. Orodhesha vitu vitano unavyopenda kufanya.
2. Taja matendo matano unayopenda kutendewa na wenzako.
3. Je, ni vitu gani usivyoweza kufanya vizuri sana?
4. Utafanya nini ili kukuza uwezo wako wa kufanya vitu hivyo?
5. Je, ni matendo gani unayotenda yanaashiria kuwa unaishi vizuri na watu wengine?

### Kazi ya kufanya

Andika majina ya watu maarufu unaowafahamu na orodhesha vipaji vyao.

### Msamiati

| | |
|---|---|
| **Kipaji** | uwezo alio nao mtu ambao humwezesha kufanya jambo vizuri |
| **Nadhifu** | enye kupendeza, safi |
| **Ustadi** | kufanya kitu kwa ujuzi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

# Tuipende shule yetu

Shule ni sehemu ya jamii ambayo huwapatia watoto malezi bora. Ili shule iwe bora inapaswa kuwa na walimu na wanafunzi bora. Shule inapaswa kuwa na madarasa, vyoo, samani, mazingira safi na vifaa vya kujifunzia. Shule yenye vitu vilivyotajwa hapo juu inavutia. Katika sura hii utajifunza matendo ya kuipenda na kujivunia shule yako. Matendo hayo hujumuisha kutunza mazingira ya shule. Vilevile, kusoma kwa bidii na kuonesha tabia njema shuleni.

## Kuifahamu shule

Miongoni mwa mambo ambayo unapaswa kuyafahamu ni vitu vinavyoitambulisha shule yako. Vitu hivyo ni mipaka ya shule, nembo ya shule na kaulimbiu. Vitu vingine vinavyotambulisha shule ni sare na wimbo wa shule.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tazama picha hii, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 1** Mazingira ya shule

**Maswali**

1. Picha hii inaonesha nini?
2. Je, ni vitu gani unavyoviona katika picha hii?
3. Eneo hili lina umuhimu gani katika jamii?
4. Je, ni mambo gani hufanyika katika eneo hili?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Wimbo

Imba wimbo huu, kisha jibu maswali.

Shule twaipenda, shule twaipenda
Shule twaipenda, shule twaipenda
Twawapenda walimu wetu, wanatufundisha vyema
Twawapenda viongozi wetu, wanatuongoza vyema
Twaipenda nembo ya shule yetu, inatutambulisha vyema
Tunazipenda sare zetu, zinatupa mwonekano bora
Taaluma, nidhamu na mazingira, hii ndio kauli mbiu yetu
Shule twaipenda, shule twaipenda
Shule twaipenda, shule twaipenda

### Maswali

1. Je, ni mambo gani yanayoitambulisha shule katika wimbo huu?
2. Je, ni mambo gani mengine yanayoitambulisha shule yako?
3. Andika wimbo wa shule yako.

### Kazi ya kufanya

Andika vitu vinavyobainisha mipaka ya shule yako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutunza mazingira ya shule

Mazingira ya shule yanajumuisha vitu vyote vilivyomo katika eneo la shule. Vitu hivyo ni majengo, viwanja vya michezo, bustani, miti na samani. Vitu vingine ni njia za shule, vyoo na vingine vingi. Ili mazingira ya shule yako yapendeze na kuvutia inakupasa kuyatunza vizuri. Kila mwanafunzi anapaswa kutunza mazingira ya shule yake. Unatakiwa kupanda miti na maua, kufanya usafi na kutupa takataka mahali panapostahili. Ni jukumu la kila mmoja kuchukua hatua ya kuzuia uchafuzi wa mazingira.

Tazama picha hii, kisha jibu maswali.



**Kielelezo namba 2** Usafi wa mazingira ya shule

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Maswali

1. Je, ni matendo gani unayoyaona kwenye picha?
2. Je, ni vitendo gani vya kutunza mazingira unavyovifanya shuleni kwako?
3. Taja faida za kusoma na kucheza kwenye mazingira safi na salama.

### Kazi ya kufanya

Shirikiana na wenzako kufanya usafi wa darasa baada ya muda wa masomo.

## Kuiletea sifa nzuri shule

Sifa nzuri ya shule inajengwa na mambo mazuri yanayofanywa na wanafunzi shuleni. Mambo kama maendeleo mazuri darasani, mazingira safi na tabia zinazofaa za wanafunzi. Juhudi za walimu huiletea sifa nzuri shule.

Soma majigambo baina ya Amani, Nuru, Upendo na Tumaini. Jibu maswali yanayofuata.

**Upendo** Mmeiona, zawadi tuliyoipata? Bila mimi kucheza mpira tusingeshinda!

**Amani** Mimi ni zaidi yako. Nimeshinda kwa kuwa na tabia njema.
Jina la shule yetu litavuma zaidi nje ya shule.

**Nuru** Mimi ni zaidi yenu. Nimeshika nafasi ya kwanza katika mitihani!

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Tumaini** Jamani ninyi nyote ni washindi! Mnastahili kupongezwa kwa kuwa mmeiletea sifa nzuri shule yetu.

**Nuru** Hapana! huwezi kulinganisha ushindi wa masomo na wa michezo!

**Amani** Ufaulu wa masomo, bila tabia nzuri ni kazi bure.

**Upendo** Msiidharau michezo kwani pia hujenga tabia nzuri.

**Tumaini** Sifa sio ufaulu wa masomo, michezo na tabia nzuri peke yake bali pia usafi. Tuipambe shule yetu na kutunza mazingira.

**Amani** Ni kweli, ushindi wa kila mmoja wetu ni ushindi wa shule.

### Maswali

1. Je, ni mambo gani yanayoileteа sifa nzuri shule uliyojifunza kwenye majigambo uliyoyasoma?
2. Ni matendo gani zaidi unayoweza kutenda ili kuiletea sifa nzuri shule yako?
3. Je, unashiriki vipi katika shughuli mbalimbali za kuiletea sifa nzuri shule yako?

### Kazi ya kufanya

Taja mambo yaliyowahi kuiletea sifa nzuri shule yako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi

1. Taja alama zilizomo katika nembo ya shule yako.
2. Andika matendo unayoyafanya kutunza mazingira ya shule yako.
3. Orodhesha vitu vinavyoitambulisha shule yako.
4. Orodhesha vitu vinavyopakana na shule yako.
5. Orodhesha mambo yanayofanyika shuleni kwako yanayokufanya uipende.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Kaulimbiu** | maneno au ujumbe unaohamasisha watu kutekeleza majukumu |
| **Majigambo** | hali ya kutoa maneno ya kujisifia au kujikweza |
| **Mazingira** | vitu vinavyotuzunguka katika eneo tunaloishi au kufanya kazi |
| **Mpaka** | mahali panapotenganisha sehemu moja na nyingine |
| **Nembo** | alama inayotambulisha kitu au sehemu kama vile shule na chama |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Tuipende nchi yetu

Katika sura hii, utajifunza kutambua na kuthamini alama za taifa. Vilevile, utaweza kutambua na kuheshimu tunu za taifa lako. Pia, utaweza kutambua na kuenzi chimbuko la nchi yako.

### Sifa za nchi yetu

Nchi yetu Tanzania ina sifa ya kuwa na amani na yenye watu waadilifu.Vilevile, watu wanapendana na kuheshimiana. Tanzania inapendeza kwa kuwa na vitu vya kuvutia. Vitu hivyo ni pamoja na milima na mbuga za wanyama. Vilevile, kuna mabonde, mito, maziwa na bahari. Watu kutoka sehemu mbalimbali duniani wanapenda kutembelea na kuishi Tanzania.

Kuna vitendo mbalimbali vinavyoonesha kuipenda nchi. Baadhi ya vitendo hivyo ni kutambua na kuthamini alama za Taifa. Vilevile, kuna tunu za Taifa na asili ya Tanzania.

Pia, inakupasa kuimba wimbo wa Taifa na nyimbo zinazoisifu Tanzania kwa unyenyekevu. Vilevile, inakupasa kuheshimu bendera ya Taifa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Wimbo

Imba wimbo huu, kisha jibu maswali.

Tanzania Tanzania, nakupenda kwa moyo wote
Nchi yangu Tanzania, jina lako ni tamu sana
Nilalapo nakuota wewe, niamkapo ni heri mama wee
Tanzania Tanzania, nakupenda kwa moyo wote.

Tanzania Tanzania, ninapokwenda safarini
Kutazama maajabu, biashara nayo makazi
Sitaweza kusahau mimi, mambo mema ya kwetu kabisa
Tanzania Tanzania, nakupenda kwa moyo wote.

Tanzania, Tanzania, watu wako ni wema sana
Nchi nyingi zakuota, nuru yako hakuna tena
Na wageni wa kukimbilia, ngome yako imara kweli wee
Tanzania Tanzania, heri yako kwa mataifa.

Nchi nzuri Tanzania, karibu kwa wasio kwao
Wenye shida na taabu, kukimbizwa na walowezi
Tanzania yawakaribisha, mpigane kiume chema wee
Tanzania Tanzania, mola awe nawe daima.

Noti za wimbo huu zinapatikana ukurasa wa 91

### Maswali

1. Ni sifa zipi za nchi ya Tanzania zinazotajwa kwenye wimbo?
2. Ni sifa gani nyingine za nchi ya Tanzania unazozifahamu?
3. Utatenda matendo gani ya kuonesha heshima unapoimba wimbo huu?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

1. Orodhesha nyimbo nyingine zinazoisifu Tanzania.
2. Andika beti zote za wimbo wa Tazama ramani.

## Kutambua alama za Taifa

Alama za Taifa ni vitu vinavyolitambulisha Taifa. Alama hizo ni bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa. Nyingine ni mwenge wa uhuru, nembo ya Taifa na mnyama (twiga). Ili kuonesha upendo kwa Taifa ni jukumu lako kutambua na kuthamini alama hizi.

Angalia picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**








**B.**













FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




C



D.




E.



**Kielelezo namba 1** Alama za Taifa

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Ni alama gani za Taifa zinazoonekana katika picha A, C, D, na E?
2. Ni vitu gani vilivyomo kwenye nembo ya Taifa?
3. Taja alama za Taifa zinazoonekana kwenye fedha hizi.
   (a) noti ya shilingi elfu moja
   (b) noti ya shilingi elfu mbili
   (c) sarafu ya shilingi hamsini
   (d) noti ya shilingi elfu kumi.
4. Bendera ya Taifa ina rangi ngapi?

## Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

1. Kuna aina kuu mbili za fedha nazo ni _______ na _________.
2. Sura ya Rais wa kwanza wa Tanzania inaonekana katika noti ya _________.
3. Rangi ya manjano katika bendera ya Taifa huwakilisha _________.
4. Maneno yanayoonekana katika ngao ya Taifa ni _________ na _______.
5. Bendera ya Taifa hupandishwa na kupepea kwenye maeneo ya
   (i) ___________
   (ii) ___________
   (iii) ___________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutambua tunu za Taifa

Vitu vingine vinavyoitambulisha nchi yetu ni tunu za Taifa. Tunu ni kitu adimu kupatikana lakini kina thamani kwa Taifa.Tunu za Taifa letu ni amani, upendo, umoja, uzalendo, mshikamano na utu. Vitu hivi ni adimu kwa nchi nyingine. Baadhi ya tunu zimetajwa katika wimbo wa Taifa. Unapoimba wimbo wa Taifa, unatakiwa usimame kwa ukakamavu.

Imba wimbo huu, kisha jibu maswali.

### Wimbo wa Taifa

Mungu ibariki Afrika
Wabariki viongozi wake
Hekima, umoja na amani
Hizi ni ngao zetu
Afrika na watu wake
Ibariki, Afrika
Ibariki, Afrika
Tubariki watoto wa Afrika.

Mungu ibariki Tanzania
Dumisha uhuru na umoja
Wake kwa waume na watoto
Mungu ibariki
Tanzania na watu wake
Ibariki, Tanzania
Ibariki, Tanzania
Tubariki watoto wa Tanzania.

Noti za wimbo huu zinapatikana ukurasa wa 92

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Ni matendo gani unayoyazingatia unapoimba wimbo wa Taifa?
2. Ni tunu gani zimetajwa katika wimbo wa Taifa?

**Kazi ya kufanya**

Chunguza eneo la shule na andika alama za Taifa utakazoziona.

## Kutambua chimbuko la Taifa la Tanzania

Nchi ya Tanzania ni muungano wa nchi ya Tanganyika na Zanzibar. Jina Tanzania limetokana na majina ya nchi hizo mbili.

Soma mazungumzo baina ya Mzee Jumbe na Fikiri, kisha jibu maswali.

**Mzee Jumbe** Je, ungependa kufahamu chimbuko la Tanzania?

**Fikiri** Ndiyo babu.

**Mzee Jumbe** Ni mambo yapi ungependa kuyafahamu kuhusu chimbuko la Tanzania?

**Fikiri** Ningependa kufahamu chimbuko la jina Tanzania. Pia, uhuru wa Tanganyika na viongozi waasisi wa Taifa letu.

**Mzee Jumbe** Nafurahishwa na udadisi wako mzuri. Jina Tanzania limetokana na majina ya nchi mbili.

**Fikiri** Ni zipi babu?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Mzee Jumbe** Nchi hizo ni Tanganyika na Zanzibar.

**Fikiri** Je, nini kilitokea kwa Tanganyika na Zanzibar?

**Mzee Jumbe** Nchi hizo ziliungana na kuunda nchi ya Tanzania.

**Fikiri** Kumbe! Ziliungana lini babu?

**Mzee Jumbe** Tanganyika na Zanzibar ziliungana tarehe 26 mwezi Aprili, mwaka 1964. Muungano huo uliunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Fikiri** Asante babu. Je, nani walikuwa viongozi wa nchi hizo wakati huo?

**Mzee Jumbe** Viongozi walikuwa Julius Nyerere wa Tanganyika na Abeid Karume wa Zanzibar.

**Fikiri** Asante sana babu kwa maelezo mazuri.

FOR ONLINE USE ONLY

### Maswali

1. Nini chimbuko la Taifa la Tanzania?
2. Nani walikuwa viongozi waasisi wa Taifa la Tanzania?
3. Jina la Taifa la Tanzania lilianza lini?
4. Mambo gani uliyojifunza katika mazungumzo haya? Je utayatumiaje katika maisha ya kila siku?

### Kazi ya kufanya

Andika mambo muhimu uliyojifunza kuhusu muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

Oanisha maneno kutoka fungu **A** na maneno kutoka fungu **B** ili kuleta maana sahihi. Andika herufi ya jibu sahihi zaidi kwenye kisanduku.

| FUNGU (A) | FUNGU (B) |
|---|---|
| 1. Mambo yanayoifanya Tanzania ivutie [ ] | A. 26 Aprili 1964 |
| 2. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar [ ] | B. Amani, upendo, umoja, uzalendo, mshikamano na utu |
| 3. Bendera ya Taifa [ ] | C. Bendera, wimbo wa Taifa, mwenge wa uhuru na mnyama twiga |
| 4. Umuhimu wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar [ ] | D. Bendera, wimbo wa Taifa, mwenge wa uhuru na mnyama tembo |
| 5. Vitambulisho vya Taifa letu [ ] | E. Ulinzi na usalama |
| | F. 24 Aprili 1964 |
| | G. Buluu, manjano, nyeusi na kijani. |

## Msamiati

**Adimu** kitu kisichopatikana kwa urahisi
**Chimbuko** mwanzo wa mtu au kitu, asili
**Muasisi** mtu aliyeanzisha jambo katika jamii
**Tunu** kitu chenye thamani sana na kisichopatikana kwa urahisi
**Udadisi** hali ya kutaka kufahamu mambo

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

# Tuithamini jamii yetu

Katika sura ya tatu ulijifunza kuhusu kulipenda taifa lako. Katika sura hii utajifunza matendo ya kuithamini jamii. Vilevile, utajifunza kujijali na kuwajali wengine. Pia, utajifunza kutunza mazingira na kujenga uhusiano mzuri na wengine.

## Kujijali na kuwajali wengine

Baadhi ya matendo ya kujijali ni kujiheshimu na kujikinga na mambo yatakayokuletea madhara. Matendo ya kuwajali wengine ni kuwapenda, kuwaheshimu na kuwasaidia. Pia, kuwajali na kuwakinga na mambo yatakayowaletea madhara.

## Kujijali

Kujijali ni kuzingatia jambo lenye manufaa katika maisha yako.

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.




**Kielelezo namba 1** Matendo ya kujijali

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Je, umejifunza nini baada ya kutazama picha hizo?
2. Je, unafahamu matendo mengine ya kujijali?

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali.

Masumbuko na Eliya ni marafiki wanaosoma katika Shule ya Msingi Chapakazi. Mara nyingi wao huenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja. Siku moja wakiwa njiani, Masumbuko aliona siafu wakikatisha katikati ya barabara. Eliya aliogopa na kupita pembeni lakini Masumbuko alielekea walipo siafu na kuwakanyaga.

Eliya alimwonya rafiki yake kuwa siafu wanaweza kumuuma lakini hakusikia, akaendelea kuwakanyaga. Wakati akifanya hivyo aliteleza na kuanguka chini pale walipo siafu. Siafu walimtambaa mwilini na kumuuma. Masumbuko alipata maumivu na kuanza kulia huku akimuita rafiki yake amsaidie. Eliya alimsogeza pembeni. Akamvua shati na kumpangusa siafu. Masumbuko alimshukuru sana rafiki yake.

**Maswali**

1. Umejifunza nini kutokana na kisa hiki?
2. Je, ni matendo gani ya kujijali uliyosoma katika kisa hiki?
3. Je, ni matendo gani ya mtu asiyejijali uliyosoma katika kisa hiki?
4. Ni matendo gani mengine ya kuwajali wengine unayoyafahamu?
5. Utamshauri nini rafiki yako mwenye tabia kama ya Masumbuko?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Andika matendo matano unayofanya kila siku yanayoonesha unajali afya na usalama wako.

## Kuwajali wengine

Unapotenda mambo mema kwa mwenzako inaonesha ni jinsi gani unamjali. Kumjali mtu mwingine ni kumtendea mambo kwa namna ambayo wewe ungependa kutendewa.

(a) Ukikutana na bibi kizee amebeba mzigo utafanya nini?

(b) Rafiki yako akiumia mpirani utafanyaje?

(c) Ukiokota begi la shule la mwanafunzi mwenzako utafanyaje?

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

B.



C.



D.



**Kielelezo namba 2** Matendo ya kuwajali wengine

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Maswali

1. Je, ni matendo gani ya kuwajali wengine unayoyaona kwenye picha hizo?
2. Ni matendo gani ya kuwajali wengine unayoyafahamu zaidi ya yaliyopo kwenye picha?
3. Utafanya nini ukikutana na hali ulizoziona kwenye picha?

### Kazi ya kufanya

Andika kisa kimoja ulichowahi kukifanya cha kuonesha kumjali mwenzako.

## Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine

Angalia matendo katika picha, kisha jibu maswali.

A.

B.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

c.



**Kielelezo namba 3** Matendo yanayojenga uhusiano mzuri

**Maswali**

1. Je, ni matendo gani unayoyaona katika picha hizi?
2. Je, umejifunza nini kutokana na matendo hayo?
5. Ni matendo gani mengine yanayojenga uhusiano mzuri?

Uhusiano mzuri hujengwa kwa kuwasiliana vyema na wenzako. Vilevile, kushirikiana nao na kuwasaidia kutatua matatizo yao hujenga uhusiano mzuri. Uhusiano mzuri husababisha watu kupendana na kuishi kwa furaha.

## Kuwasiliana vyema darasani na nje ya darasa

Katika maisha ya kila siku, tunawasiliana kwa kupeana taarifa. Tunasalimiana, tunaeleza tunavyojisikia na kutoa maoni. Baadhi ya maneno tunayotumia kuwasiliana na wenzetu ni asante, naomba na pole.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Nyamizi ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Umoja. Yeye ni mwanafunzi mwenye tabia njema. Amekuwa akitimiza wajibu wake shuleni na nyumbani. Mara nyingi anapokuwa hajaelewa walichojifunza darasani, huwaomba wanafunzi wenzake wamsaidie. Anaposaidiwa husema asante. Anapowakosea wenzake husema samahani. Pia, huwapa pole wenzake wanapopata matatizo. Kutokana na tabia hiyo, Nyamizi amepata marafiki wengi shuleni.

**Maswali**

1. Umejifunza nini kutokana na kisa hiki?
2. Ni maneno gani yanayoonesha lugha inayofaa katika habari hii?
3. Je, ni sifa gani zinazomfanya Nyamizi awe na marafiki wengi?
4. Ni njia gani nyingine za kujenga uhusiano mzuri unazozifahamu?

## Kushiriki kutatua matatizo ya watu wengine

Unaposhiriki kutatua matatizo ya wenzako unajenga upendo na uhusiano mzuri baina yenu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**



**B.**



FOR ONLINE USE ONLY

C.



**Kielelezo namba 4** Matendo ya kushiriki kutatua matatizo ya wengine

**Maswali**

1. Ni matendo gani ya kutatua matatizo ya wengine yanayooneshwa katika picha A, B na C?
2. Ni matendo gani mengine unayoyafanya kutatua matatizo ya wengine?

## Kutunza mazingira

Kutunza mazingira ni kuyalinda na kuyahudumia ili yavutie na kupendeza. Ni pamoja na kufanya usafi na kutupa takataka mahali panapostahili.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutambua mazingira yanayokuzunguka

Soma mazungumzo haya, kisha jibu maswali.

| | |
|---|---|
| **Asha** | Shikamoo, dada Mwanaidi. |
| **Mwanaidi** | Marahaba, mdogo wangu. |
| **Asha** | Dada, nini maana ya mazingira? |
| **Mwanaidi** | Kwani hamkufundishwa shuleni? |
| **Asha** | Tumefundishwa lakini sikumwelewa vizuri mwalimu. |
| **Mwanaidi** | Sawa, mazingira ni kila kitu kinachotuzunguka. Mfano, hewa, watu na mimea. |
| **Asha** | Je, ndege na wanyama nao ni sehemu ya mazingira? |
| **Mwanaidi** | Ndiyo, nao ni sehemu ya mazingira. |
| **Asha** | Nashukuru dada yangu. Sasa nimefahamu maana ya mazingira. |
| **Mwanaidi** | Nami nimefurahishwa na shauku yako ya kutaka kufahamu. |

### Maswali

1. Kutokana na habari uliyosoma, neno mazingira lina maana gani?
2. Ni vitu gani vinaunda mazingira kutokana na mazungumzo?
3. Ni vitu gani vingine vinaunda mazingira zaidi ya vile alivyovitaja Asha?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

1. Orodhesha kazi tatu zinazofanywa kwa lengo la kutunza mazingira ya nyumbani.
2. Orodhesha kazi tatu zinazofanywa kwa lengo la kutunza mazingira ya shule.

## Kuthamini mimea na wanyama

Tunatakiwa kutunza na kuthamini mazingira ili wanyama wakue vizuri na mimea istawi.

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B.**



**C.**



**Kielelezo namba 5** Matendo ya kuthamini mimea na wanyama

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Maswali

1. Umeona nini katika picha hizi?
2. Je, ni picha zipi zinazoonesha matendo ya kuthamini wanyama?
3. Ni picha ipi inaonesha tendo la kuthamini mimea?
4. Ni matendo gani mengine unayoyafahamu ya kuthamini wanyama na mimea?

### Kazi ya kufanya

Tengeneza ratiba yako ya wiki inayoonesha matendo ya kutunza mazingira ya nyumbani. Jitahidi kuifuata ratiba hiyo.

## Kutunza vyanzo vya maji

Maji ni muhimu kwa maisha ya watu, mimea na wanyama. Maji yanatokana na vyanzo kama vile mvua, mito, chemchemi, maziwa na bahari.

Maji ni rasilimali muhimu hivyo inatupasa kuyatumia kwa uangalifu na kuyatunza. Matendo yanayochafua maji ni kuoga, kufua na kujisaidia kwenye vyanzo vyake. Vilevile, maji yanaharibiwa kutokana na vitendo vya kunywesha mifugo na kutupa takataka.

Aidha, tunashauriwa tusitumbukize vitu vyenye sumu kwenye maji. Pia, kuacha maji yapotee bila matumizi ni uharibifu wa maji.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia picha hizi, kisha jibu maswali.




**Kielelezo namba 6** Matendo yanayoonesha utunzaji na uharibifu wa vyanzo vya maji.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Ni matendo gani yanayoonekana katika picha A, B, C na D?
2. Ni tendo gani la utunzaji wa chanzo cha maji linaloonekana katika picha?
3. Ni matendo gani ya uharibifu wa vyanzo vya maji yanayoonekana katika picha?
4. Ni matendo gani mengine ya utunzaji wa maji unayoyafahamu?
5. Ni hasara gani zinapatikana kwa kuharibu vyanzo vya maji?
6. Ni matendo gani utafanya ili kuonesha kuwa unaithamini jamii yako?

## Kazi ya kufanya

Andika mambo mawili yanayoashiria uharibifu wa vyanzo vya maji pale unapoishi.

## Zoezi

1. Taja njia utakazotumia kumsaidia mtoto aliyeanguka darasani.
2. Orodhesha njia tatu utakazotumia katika kujenga uhusiano mzuri na watu wengine.
3. Taja matendo matatu yanayoharibu vyanzo vya maji.
4. Andika kisa kimoja ulichowahi kushiriki kumsaidia mwanafunzi mwenzako kutatua tatizo lake.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Chagua maneno sahihi kutoka **safu B** na ujaze nafasi zilizoachwa wazi katika **safu A.**

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| **Mfano** Pole utapona rafiki yangu. | Nashukuru |
| (i)..........niazime kalamu. | Samahani |
| (ii).........mwalimu sitarudia tena. | Naomba |
| (iii).........umenisaidia kweli! | Pole |
| (iv).........naomba kupita. | Asante |
| | Tafadhali |
| | Hebu |
| | Sawa |

## Msamiati

**Chemchemi** maji yanayotoka ardhini

**Kisa** masimulizi ya tukio la kweli lililotokea au maelezo ya hadithi za kubuni

**Kujali** kuzingatia mambo muhimu katika maisha

**Kuthamini** tia maanani, heshimu

**Rasilimali** mali alizonazo mtu au jamii

**Shauku** hamu ya kutaka kujua jambo

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

# Tuwajibike

Sura ya nne ulijifunza matendo ya kuithamini jamii.Katika sura ya tano utajifunza kuwajibika, kujenga nidhamu binafsi na kulinda rasilimali. Vilevile, utajifunza kutekeleza na kusimamia majukumu yako. Pia, utajifunza kushirikiana na watu wengine katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

## Kulinda rasilimali za jamii

Rasilimali ni vitu vinavyoweza kutumika kutuletea maendeleo. Hivyo ni wajibu wa kila mmoja kulinda rasilimali zinazotuzunguka katika mazingira yetu.

## Kutambua rasilimali zilizopo katika mazingira yetu

Angalia picha hizi, kisha jibu maswali.

A.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**B.**



**Kielelezo namba 1** Rasilimali zilizopo katika mazingira ya shule

**Maswali**

1. Unaona nini katika picha A na B ?
2. Je, ni rasilimali gani zinazoonekana katika picha A?
3. Je, ni rasilimali gani zinaonekana katika picha B?
4. Ni rasilimali gani zinapatikana katika shule yako?

Baadhi ya vitu vilivyopo shuleni ni majengo, madawati na viwanja vya michezo. Pia, kuna miti, maji, vitabu, umeme na vifaa vya michezo. Vitu hivi vinavyopatikana shuleni ni rasilimali za shule.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Andika rasilimali zote zilizopo shuleni kwako.

## Kutunza rasilimali zilizopo katika mazingira yanayokuzunguka

Kutunza rasilimali ni kuzihifadhi ili zidumu na kuwanufaisha watu wote.

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Baraka na Sara ni viranja wa ulinzi katika Shule ya Msingi Kisiwani. Kila asubuhi, Baraka hukagua usalama wa rasilimali katika madarasa yote. Sara naye hukagua vyoo, mabomba ya maji na vifaa vya usafi. Hufanya hivyo ili kuhakikisha usalama wake. Siku moja Baraka alibaini uharibifu wa viti vitatu katika darasa la tatu. Baraka alimhoji kiongozi wa darasa ili kujua aliyehusika na uharibifu huo. Baraka alijulishwa kuwa Masero ndiye aliyeharibu viti hivyo. Baraka aliamua kulifikisha suala hilo kwa mwalimu wa darasa.

Mwalimu alimwandikia barua mzazi wa Masero akimtaka afike shuleni. Sababu za kumwalika mzazi wa Masero shuleni ni kuzungumzia uharibifu alioufanya Masero. Baada ya majadiliano, mzazi alitakiwa kulipa gharama za ukarabati wa madawati yaliyoharibika. Mwalimu alimwonya Masero. Akawaambia wanafunzi wote kuwa, wanapaswa kuwajibika kutunza rasilimali zote za shule.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Umejifunza nini katika habari hii?
2. Ni vitendo gani vinavyoonesha kutunza rasilimali za shule vilivyotajwa katika habari hii?
3. Je, ni watu gani wanawajibu wa kutunza rasilimali za shule?
4. Ni vitendo gani utavifanya ili kutunza rasilimali za shule yako?

**Kazi ya kufanya**

Orodhesha rasilimali za shule na andika kila rasilimali inakotunzwa. Kwa mfano,

i. redio – ofisini kwa mwalimu mkuu

ii. vitabu – maktaba

## Kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

A.



B.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

C.



D.



E.



**Kielelezo namba 2** Wanafunzi wakitimiza majukumu ya nyumbani na shuleni

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Unaona nini katika picha A, B, C, D na E?
2. Je, ni majukumu gani mengine unayopaswa kutimiza nyumbani na shuleni?
3. Je, kuna faida gani za kutimiza majukumu yako?

**Kazi ya kufanya**

Tengeneza ratiba ya kazi utakazofanya nyumbani kwa wiki nzima.

## Kusimamia utekelezaji wa majukumu shuleni na nyumbani

Ili kusimamia na kutekeleza majukumu ni vyema kutambua kazi za kufanya. Hivyo, ni vizuri kuorodhesha kazi na kuziwekea utaratibu wa kuzitekeleza.

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Joshua ni kiranja wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Ukombozi. Hupanga ratiba ya kufanya usafi wa darasa kila wiki. Pia huhamasisha wanafunzi wote kupenda kufanya usafi wa darasa lao. Joshua huandika majina ya wanafunzi wanaofanya usafi vizuri na kuyabandika ukutani. Wanafunzi wanaofanya usafi vizuri hupongezwa na wenzao kwa kupigiwa makofi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vilevile, Joshua husimamia kazi za darasani, huzikusanya na kumpelekea mwalimu wa somo. Kutokana na uhodari wa Joshua aliteuliwa kuwa kiranja wa mazingira shuleni.

**Maswali**

1. Je, Joshua ana sifa gani?
2. Kwa nini Joshua aliteuliwa kuwa kiranja wa mazingira?
3. Ni mambo gani unayojifunza kutoka kwa Joshua?

Jukumu la kusimamia kazi za shuleni na nyumbani ni la kila mtu. Jukumu hilo sio la viongozi au wazazi pekee. Kila mtu anapaswa kujisimamia mwenyewe na kusimamia wengine pale inapobidi.

**Kazi ya kufanya**

Andika mambo manne utakayoyafanya kusimamia wenzako endapo utachaguliwa kuwa kiranja wa darasa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Matendo ya ushirikiano

Angalia picha zifuatazo, kisha jibu maswali.

**A.**



**B.**




**C.**



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**D.**



**Kielelezo namba 3** Wanafunzi wakifanya matendo ya ushirikiano

**Maswali**

1. Ni matendo gani ya ushirikiano unayoyaona katika picha A, B, C na D?
2. Je, ni matendo gani mengine ya ushirikiano unayoyafahamu?
3. Je, kuna faida gani za kushirikiana na wenzako katika kufanya kazi mbalimbali?

Wanafunzi hushirikiana katika masomo, usafi, michezo na klabu za masomo. Ushirikiano hujenga urafiki miongoni mwetu na kutuwezesha kufanya kazi vizuri. Ili tufaulu masomo yetu inatupasa kushirikiana wakati wa kujifunza.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Andika mambo matano ambayo unahitaji kushirikiana na wenzako shuleni.

## Kukosoa na kukubali kukosolewa

Kukosoa ni kumwambia mtu makosa yake. Kukubali kukosolewa ni kukubali kuambiwa upungufu wako.

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Maira ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Iringo.Wakati wa mapumziko hujadili mambo mbalimbali na wanafunzi wenzake. Maira aliwaambia wenzake Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanzania ni Edward Sokoine. Amoni alimkosoa kwa kusema kuwa, Waziri Mkuu wa kwanza ni Rashidi Kawawa. Maira hakukubali akamdhihaki mwenzake. Siku iliyofuata, mwalimu wa somo la Uraia na Maadili aliingia darasani. Mwanafunzi mwenzao aitwaye Salma ambaye alishuhudia mjadala wao aliuliza swali. Mazungumzo yalienda hivi.

**Salma** Mwalimu, eti Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanzania anaitwa nani?

**Mwalimu** Wanafunzi, nani anaweza kujibu swali hili?

**Amoni** Anaitwa Rashidi Kawawa.

**Maira** Si kweli, mwalimu. Anaitwa Edward Sokoine.

**Mwalimu** Jibu sahihi ni Rashid Kawawa.

**Maira** Nashukuru, mwalimu. Nakubaliana na jibu lako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Maswali

1. Ni tabia gani aliyoonesha Amoni?
2. Umejifunza nini kutokana na tabia ya Maira?
3. Je, unapata faida gani ukikubali kukosolewa?

### Kazi ya kufanya

Orodhesha matukio mawili ya kukosolewa unayoyakumbuka.

### Zoezi

1. Taja matendo matatu yanayoonesha kuwa unawajibika kutunza rasilimali za shule.
2. Taja matendo matatu ambayo mtoto mwenye nidhamu binafsi huyafanya shuleni na nyumbani.
3. Eleza majukumu ya kiongozi wa darasa.

### Msamiati

**Kudhihaki** kudharau hoja ya mtu

**Kujituma** kufanya jambo jema bila kusimamiwa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

# Tuwe wastahimilivu

Sura iliyopita ulijifunza matendo ya uwajibikaji. Katika sura hii utajifunza namna ya kujenga tabia ya uvumilivu. Pia, utajifunza kuhimili vikwazo ili kufikia malengo.

## Kuvumilia katika maisha ya kila siku

Unapaswa kuwavumilia watu wengine wenye tabia tofauti na yako. Pia, unatakiwa kuwa mvumilivu unapokosa vitu unavyohitaji katika maisha ya kila siku.

## Kuwakubali watu wengine

Binadamu tunatofautiana kwa maumbile na mawazo. Wapo wenye ulemavu wa viungo na akili. Pia, wapo wenye mawazo tofauti na yako. Unapaswa kuwavumilia na kuwakubali watu wengine wenye mawazo na maumbile tofauti.

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Robi, Juma na Sayi wanasoma katika Shule ya Msingi Mwakaleli. Siku moja Robi alimcheka Juma alipokuwa anawasimulia hadithi. Sababu ya kumcheka Juma ilitokana na kuongea kwa kigugumizi. Sayi hakupenda hiyo tabia kwani ilimfanya Juma kuogopa kuongea mbele ya wenzake. Sayi alimwita Robi akamwambia, “usimcheke tena Juma, kwani yeye hakupenda awe hivyo”. Robi alikwenda kumwomba Juma msamaha. Juma alimsamehe Robi na waliendelea kuwa marafiki.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Katika habari hii, Robi alionesha tabia ya aina gani?
2. Ni tabia gani nzuri tunayojifunza kutoka kwa Sayi?
3. Ungekuwa katika nafasi ya Juma, ungechukua hatua gani?
4. Je, ni matendo gani mengine unayoyafahamu ya kuwakubali wengine?

Angalia picha hizi kisha jibu maswali.

**A.**



**B.**




**Kielelezo namba 1** Matendo ya kuwakubali na kutowakubali watu wengine

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Ni tendo gani la kuwakubali watu wengine linalooneshwa katika picha?
2. Ni tendo gani la kutowakubali watu wengine linalooneshwa katika picha?
3. Ni matendo gani mengine ya kuwakubali watu wengine unayoyafahamu?

**Kazi ya kufanya**

Eleza utakavyomsaidia mwanafunzi mwenye ulemavu wa miguu aweze kukaa kwenye dawati.

## Kuwavumilia wengine

Tunaishi pamoja na watu wenye tabia tofauti katika jamii. Zipo tabia zinazofaa na zisizofaa. Uvumilivu utakusaidia kuishi vyema na watu wenye tabia mbalimbali.

Tazama picha hii na kusoma, kisha jibu maswali.




**Kielelezo namba 2** Matendo ya kuwavumilia wengine

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Je, ni tabia ipi aliyoonesha John?
2. Kama wewe ungekuwa John ungefanyaje?
3. Ni matendo gani mengine ya uvumilivu unayoweza kuyafanya?

Mwanafunzi, ni vyema kujifunza namna ya kuwavumilia wengine uwapo shuleni na nyumbani. Ukiwa mvumilivu utaweza kujifunza vyema shuleni na kufanikiwa katika maisha yako.

**Kazi ya kufanya**

Orodhesha matendo ya uvumilivu utakayoyafanya nyumbani na shuleni.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kutumia lugha inayofaa pindi unapokosewa

Ukitumia lugha inayofaa kuwasiliana na mwenzako utaheshimika, utasikilizwa na utaepuka ugomvi. Unapokosolewa ni vema uwe na hekima, kwani hekima itakujenga. Pia hekima itakuepusha na matatizo.

Soma majadiliano haya kati ya Lomayani na Hadija, kisha jibu maswali.

| | |
|---|---|
| **Lomayani** | Habari yako, dada Hadija? |
| **Hadija** | Nzuri. |
| **Lomayani** | Nasikia siku hizi wewe ndio namba moja |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

darasani.

**Hadija** Ndiyo, kaka. Kwani wewe ni namba ngapi darasani kwako?

**Lomayani** Nipo katikati, si wa kwanza wala wa mwisho.

**Hadija** Hahahaa! Nasikia ulipata alama sifuri katika mtihani wa Hisabati.

**Lomayani** Sasa ndio unicheke?

**Hadija** Hahaa! Nakuonea huruma. Hivi utabebaje hiyo sifuri?

**Lomayani** Mimi sipendi unavyonicheka. Najisikia vibaya.

**Hadija** Basi jitahidi ufaulu ili nisikucheke tena.

### Maswali

1. Ni maneno gani yanayoonesha mmoja kumkosea mwenzake?
2. Je, ni maneno gani yanayoonesha uvumilivu katika majadiliano hayo?
3. Orodhesha matukio mawili ya kukosewa uliyofanyiwa.
4. Je, ulifanya nini kwenye kila tukio?
5. Nini kilitokea baadaye?
6. Kuanzia sasa unapokosewa utafanya nini?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuhimili vikwazo ili kufikia malengo

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Hamisi ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Ushindi. Alifanya mitihani muhula wa kwanza na kuwa mwanafunzi wa tano darasani kwao. Hamisi aliongeza bidii katika masomo yake ili awe katika nafasi ya kwanza. Alijiwekea ratiba ya kusoma nyumbani na kuifuata. Alizingatia utaratibu wa shule na kufanya kazi zake zote kwa wakati. Mara nyingi Hamisi hukosa vitabu vya kujisomea. Hivyo huazima vitabu kwa wanafunzi wa shule za jirani. Hamisi hutembea umbali mrefu kwenda shule za jirani ili kufanya mitihani ya kujipima. Hatimaye, Hamisi alifaulu na kufikia malengo yake.

### Maswali

1. Ni vikwazo vipi alivyokutana navyo Hamisi?
2. Je, Hamisi aliwezaje kufikia malengo yake licha ya vikwazo hivyo?
3. Je, unafikiri tabia ya Hamisi inafaa kuigwa? Kwa nini?

### Kazi ya kufanya

1. Andika lengo unalotaka kulifikia unapojifunza Uraia na Maadili.
2. Bainisha vikwazo unavyofikiri utakabiliana navyo katika kufikia lengo lako.
3. Eleza jinsi utakavyokabiliana na vikwazo hivyo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuvumilia katika kudadisi mambo

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali.

Salim ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Wami. Salim na wazazi wake wanaishi karibu na milima ya Uluguru. Mara nyingi huona kitu cheupe katikati ya mlima. Siku moja Salim alitamani kujua kitu alichokuwa akikiona mlimani. Hivyo, alimfuata rafiki yake Kobelo na kumsimulia kuhusu kitu anachokiona mlimani. Walikubaliana kuwa wapande mlima kwenda kujionea. Walianza safari ya kupanda mlima asubuhi. Walitembea kwa muda mrefu sana hadi wakachoka. Kobelo alimshauri Salim wasitishe safari yao. Salim hakukubali na alimshawishi rafiki yake waendelee na safari yao.

Mvua ilianza kunyesha, kukawa na utelezi uliosababisha watembee kwa taabu. Pamoja na hali hiyo waliendelea na safari yao. Hatimaye walifika mahali palipokuwa na maporomoko ya maji yaliyokuwa yanaenda kwa kasi. Salim akatahamaki, "Ahaa! kumbe kitu nilichokuwa nakiona ni haya maporomoko ya maji?" Pia aligundua kuwa maji hayo ndio chanzo cha mto. Mto huo ulipita karibu na nyumbani kwao. Walirudi nyumbani kwa furaha na kuwaeleza wazazi wao kile walichokiona.

### Maswali

1. Ni matendo gani ya udadisi yaliyooneshwa na Salim?
2. Ni matendo gani ya uvumilivu yaliyooneshwa na Salim?
3. Ni tabia gani iliyooneshwa na Kobelo?
4. Unajifunza nini kutokana na kisa hiki?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya kufanya

Je, somo gani ni gumu kwako? Taja vikwazo unavyopata katika kujifunza somo hilo. Kisha andika matendo ya uvumilivu unayofanya katika kujifunza somo hilo.

### Zoezi

Andika **ndiyo** kwenye sentensi sahihi na **hapana** kwenye sentensi isiyo sahihi.

1. Ili tufikie malengo yetu inatupasa kuhimili vikwazo.
2. Ukiwa mvumilivu hutaweza kujifunza vyema na kufanikiwa kimaisha.
3. Tunapaswa kuwakubali watu wenye mawazo na maumbile tofauti na yetu.
4. Ukifanya kazi na kumaliza kwa wakati utakuwa mtiifu.
5. Sio vizuri kuzungumza na mwenzako kwa lugha nzuri.

FOR ONLINE USE ONLY

### Msamiati

**Kuhimili** kuvumilia, ustahimilivu

**Malengo** nia ya kufanya kitu

**Kikwazo** kizuizi kinachomzuia mtu kufanya jambo

**Ulemavu** kuwa na kasoro ya kimaumbile

**Hekima** busara au maarifa ya hali ya juu

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Tuwe waadilifu

Katika sura ya sita ulijifunza namna ya kujenga tabia ya uvumilivu. Sura hii ya saba itakuwezesha kujifunza matendo ya uadilifu. Matendo hayo ni uaminifu, ukweli, uwazi na kutenda haki. Uadilifu ni hali ya kuishi kwa kufuata maadili ya jamii.

### Kujenga tabia ya uaminifu

Uaminifu unajengwa kwa kutenda matendo kama vile kutimiza ahadi na kusema ukweli. Vilevile, kutunza siri, kufichua uovu na kutunza mali uliyokabidhiwa. Pia, uaminifu unaonekana pale mtu anapozingatia malengo yake ikiwemo ratiba binafsi.

Chunguza matendo haya.

(a) Mwanafunzi amerudisha kitabu alichoazima kwa mwalimu kwa wakati.

(b) Mtoto ametoa ushahidi juu ya wizi wa fedha alioufanya mwenzake.

(c) Mtoto ametoa taarifa kwa mama yake kuwa amevunja sahani.

Bila shaka umejifunza kuwa matendo hayo hujenga tabia ya uaminifu. Ni muhimu kuwa mwaminifu katika maisha yako.

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali.

Hoza na Yohana ni wanafunzi wa darasa la tatu. Siku moja Hoza

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na Yohana walikuwa wakitembea njiani. Walimwona Mzee Juma akiendesha baiskeli yake na mara alipowapita alidondosha pochi yake. Hoza akaiokota ile pochi na kumwonyesha Yohana. Yohana akaipekua na kukuta fedha ndani yake. Akamshauri Hoza wagawane. Hoza akakataa. Alichukua ile pochi na kumkimbilia Mzee Juma na akampa pochi yake. Mzee Juma akashukuru na kumpa zawadi ya shilingi elfu kumi. Hoza akakataa kuichukua ile hela. Yohana alimlaumu sana Hoza kwa kurudisha zile fedha.

Siku iliyofuata, Hoza na Yohana walienda dukani kununua kalamu na daftari. Walipofika dukani, Hoza aligundua kuwa ana fedha pungufu. Akamwomba muuza duka ampatie kwa ahadi ya kumlipa siku iliyofuata. Mara Mzee Juma akatokea.

Mzee Juma akamuuliza, "Hoza umekuja kununua nini?" Muuza duka akasema wanahitaji kalamu na daftari lakini wanataka kukopa. "Ooh! mwanangu Hoza nitakulipia," alisema Mzee Juma.

**Maswali**

1. Ni matendo gani ya uaminifu yaliyotendwa na Hoza?
2. Ni matendo gani ya kukosa uaminifu yaliyofanywa na Yohana?
3. Unadhani kwa nini Mzee Juma alifurahi kumlipia Hoza?
4. Ni faida gani aliyopata Hoza kwa kuwa mwaminifu?

**Kazi ya kufanya**

Eleza faida za matendo ya uaminifu unayoyaona katika jamii inayokuzunguka.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kutambua matendo ya kukosa uaminifu

Katika maisha, matendo ya ukosefu wa uaminifu yanajitokeza mara nyingi. Je, umeshawahi kukutana na mtu asiye mwaminifu?

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali.

Wanafunzi wa Shule ya Msingi Rebu walipanga kununua mpira wa miguu. Walichangisha fedha ili watimize lengo lao. Wakamchagua Kimune awe anatunza fedha. Walifanikiwa kupata fedha za kutosha. Siku ya Jumamosi, Kimune na Duda waliagizwa kwenda kununua mpira mnadani. Walipofika mnadani walikubaliana wakachunguze bei kabla ya kununua. Baada ya kutembea kidogo walikutana na watu wanaocheza kamari ya karata. Kimune alivutiwa na mchezo huo. Alimshawishi Duda wacheze ili kuzalisha ile fedha. Duda alikataa kwa kusema "Hii fedha ikiliwa tutawaambia nini wenzetu?" Kimune hakumtii, akaanza kucheza. Wakati Kimune akiendelea kucheza, Duda akaondoka kwenda kuwataarifu wenzake. Kimune alipocheza mara ya kwanza alibahatika kushinda, akanogewa. Mara nyingine zote aliliwa. Ooh! Kutahamaki fedha yote ilikwisha. Hakuwa na fedha ya kununua mpira tena. Kimune akaanza kulia akijutia uamuzi wake.

FOR ONLINE USE ONLY

### Maswali

1. Unajifunza nini kutokana na kisa hiki?
2. Je, mambo kama haya yanatokea katika jamii yako?
3. Ni hasara gani zilizopatikana kutokana na kucheza kamari?

### Kazi ya kufanya

Andika matendo ya kukosa uaminifu unayoyafahamu.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuwa muwazi na mkweli

Ukweli na uwazi ni mambo ya msingi katika maisha. Kutokuwa mkweli na muwazi kunaweza kusababisha matatizo makubwa. Matatizo hayo ni kama ugomvi, kutoaminika, uvunjifu wa amani au kukosa amani.

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Mcheku na Sara ni wanafunzi katika Shule ya Msingi Kideka. Wakati wa mapumziko walienda kucheza kwenye kichaka karibu na shule yao. Walikuwa wanaokota kokoto kwa ajili ya kucheza mchezo wa “kwangu kwako”. Mara Mcheku alipiga kelele kuashiria maumivu makali. Sara aliuliza, “Umepatwa na nini?” Mcheku alimwambia kuwa ameng’atwa na nyoka. Wote walikimbia kurudi shuleni huku Mcheku akiugulia maumivu. Waliogopa kusema kwa kuwa walikatazwa kucheza kwenye kichaka hicho.

Kengele ya kuingia darasani iligongwa. Wakaingia darasani huku wakiwa na woga sana. Taratibu sumu ya nyoka ilienea mwilini mwa Mcheku na kumfanya apoteze fahamu. Wanafunzi waliokaa naye wakatoa taarifa kwa mwalimu. Mwalimu hakujua nini kilitokea. Alishirikiana na wanafunzi kumpeleka Mcheku hospitalini.

Huko hospitalini, hali ya Mcheku ilizidi kuwa mbaya. Hakuna aliyejua kilichompata Mcheku isipokuwa Sara. Hatimaye Sara aliamua kumsimulia mwalimu mkuu kilichompata Mcheku. Mwalimu mkuu alitoka haraka kwenda hospitalini. Aliwaeleza madaktari tatizo la Mcheku. Mcheku alitibiwa na kupata nafuu. Mwalimu mkuu alirudi shuleni akaitisha mkutano wa wanafunzi wote. Akawapa taarifa za ugonjwa wa Mcheku.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Unajifunza nini kutokana na kisa hiki?
2. Je, ni mambo gani yaliyotokea katika habari hii?
3. Unawashauri nini wanafunzi wenye tabia kama za Sara na Mcheku?
4. Ukipatwa na jambo kama hili utafanya nini?

Ni vyema watoto kuzungumza na wazazi, walezi na walimu kwa uwazi. Ni vyema pia kujua mambo wanayofanya au kufanyiwa watoto. Kuwa muwazi na mkweli kutakusaidia kutatua tatizo ulilonalo kwa wakati.

**Kazi ya kufanya**

Andika faida tano za kuwa muwazi na mkweli.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kutambua wajibu na haki za watoto

(a) Wewe kama mwanafunzi na mtoto una haki na wajibu gani?

(b) Je, ni mambo gani ungependa wazazi wako wakufanyie?

(c) Je, ni mambo gani usingependa ufanyiwe na wazazi au watu wengine?

(d) Je, ni mambo gani unapaswa kuyafanya shuleni na nyumbani?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Watoto wana haki zao. Baadhi ya haki za watoto ni kupendwa na kupewa elimu bora. Pia watoto wana haki ya kupata huduma za afya. Vilevile, ni haki yao kula chakula bora, kulindwa na kusikilizwa. Hata hivyo watoto wanatakiwa kutimiza wajibu wao. Wajibu wao ni kusoma kwa bidii, kuwapenda wengine na kutunza afya zao.Watoto wana wajibu pia wa kutii wazazi na walimu na kuwasaidia wengine.

Chunguza matendo yafuatayo yanayoonesha haki na wajibu wa mtoto. Weka alama ya (✓) kwenye kisanduku utakachochagua. Angalia mfano uliopewa namba 1 na 2.

| **Na.** | **Matendo** | **Haki** | **Wajibu** |
|---|---|---|---|
| 1. | Kujifunza kutokana na makosa | | ✓ |
| 2. | Kuishi katika nyumba nzuri | ✓ | |
| 3. | Kushirikishwa kufanya maamuzi | | |
| 4. | Kuthamini watu wenye ulemavu | | |
| 5. | Kucheza kwa furaha | | |
| 6. | Kupata malezi bora | | |
| 7. | Kuwasikiliza wengine | | |
| 8. | Kupewa jina zuri | | |
| 9. | Kulindwa | | |
| 10. | Kufanya kazi zinazolingana na uwezo wao | | |
| 11. | Kupata elimu bora | | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia picha hizi, kisha jibu maswali.

A.



B.



C.




D.



**Kielelezo namba 1** Matendo yanayoonesha kutendewa haki na kutekeleza wajibu.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Unaona nini katika picha A, B, C na D?
2. Je, mambo kama hayo yanafanyika katika jamii yako?
3. Ni matendo yapi yanaonesha watoto kutendewa haki zao?
4. Je, ni haki gani unazopatiwa nyumbani na shuleni?
5. Usipopewa haki yako nyumbani utafanya nini?
6. Usipopewa haki yako shuleni utafanya nini?

**Kazi ya kufanya**

Andika kazi tano unazofanya ukiwa
(a) shuleni
(b) nyumbani

## Kutambua matendo yanayokiuka haki za watoto

Watoto wanatakiwa kupendwa na kulindwa na watu wote ili wakue vizuri. Ni makosa kuwatesa watoto. Haifai kufanya kazi ngumu na zenye athari kwa afya yao. Kwa mfano, mtoto hapaswi kuponda kokoto na kubeba mizigo mizito na kupewa adhabu kali ya kuchapwa viboko.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya kufanya

Orodhesha matendo yanayokiuka haki za mtoto katika mazingira yanayokuzunguka.

### Zoezi

1. Orodhesha matendo ya uaminifu unayoyatenda shuleni na nyumbani.
2. Taja matendo yasiyo ya uaminifu wanayofanya watoto shuleni na nyumbani.
3. Orodhesha haki za watoto unazozifahamu.
4. Eleza wajibu wa mtoto nyumbani na shuleni.

FOR ONLINE USE ONLY

### Msamiati

**Haki** jambo ambalo mtu anastahili au kitu anachostahili kuwa nacho

**Wajibu** jambo linalomlazimu mtu kulitimiza

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Tudumishe amani

Katika sura hii utajifunza jinsi ya kuishi kwa amani. Aidha, unaweza kushirikiana na watu wengine katika jamii. Utajifunza jinsi ya kuishi na watu wenye asili tofauti. Vilevile, utajifunza kuheshimu tofauti za kiutamaduni na kujenga urafiki unaofaa na watu.

Amani inaweza kutafsiriwa kuwa ni hali ya utulivu isiyokuwa na fujo au vita. Vilevile, amani inapatikana katika hali ya usalama na utulivu.

Ni vyema kutambua kuwa tunaishi na watu wenye asili tofauti na sisi. Watu hao tunashirikiana nao wakati wote tukisoma na kufanya kazi. Vilevile, tunashirikiana wakati wa kusafiri, kucheza na kusherehekea pamoja.

### Kuishi na watu wenye asili na tamaduni tofauti

Nchi yetu ina watu wa makabila mbalimbali kutoka mikoa mbalimbali. Watu hao wanatofautiana katika lugha, mavazi, vyakula na makazi. Pia tunaishi na wageni kutoka mataifa mengine kama Wazungu, Wahindi na Waarabu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**



**B.**



**Kielelezo namba 1** Asili na tamaduni mbalimbali



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Unaona nini katika picha A na B ?
2. Umejifunza nini kutokana na picha hizi?
3. Je, umewahi kuishi na watu wenye asili tofauti na yako?
4. Je, kuna mambo ambayo uliyaona tofauti na ya jamii yako?

Soma majigambo baina ya Mhehe, Mnyakyusa na Mnyamwezi, kisha jibu maswali.

| | |
|---|---|
| **Mhehe** | Wahehe tunatokea Iringa yaani tunaringa! |
| **Mnyakyusa** | Mnaringia nini? |
| **Mhehe** | Wahehe ndio kitovu cha Watanzania. Tunajivunia Kalenga. |
| **Mnyamwezi** | We! Mhehe tena unyamaze kabisa. Kitovu cha Watanzania ni Tabora. |
| **Mhehe** | Tulipigana na Mjerumani tukaua askari wake wengi kuliko kabila lolote. |
| **Mnyakyusa** | Sisi hatukupigana na mkoloni wala Mwarabu. Wote walituogopa. |
| **Mnyamwezi** | Ngome kuu ya Tanzania ni Tabora nyumbani kwa Isike na Mirambo. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Je, unafahamu makabila gani mengine ya Tanzania zaidi ya yaliyotajwa katika majigambo?
2. Je, tunapata faida gani watu wa makabila tofauti wakiishi pamoja kwa amani?
3. Unajifunza nini kutokana na majigambo uliyosoma?

## Kazi ya kufanya

Waombe wanafunzi wenzako wataje makabila yao na mikoa wanayotoka. Waambie waandike makabila yao katika madaftari yao.

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**



**B.**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 2** Matendo ya ushirikiano baina ya watu wenye asili tofauti

FOR ONLINE USE ONLY

### Maswali

1. Ni matendo gani unayoyaona kwenye picha A na B ?
2. Je, unajifunza nini kutokana na picha hizo?
3. Je, ni jinsi gani unashirikiana na watu wenye asili tofauti na yako?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Tumaini na Mkakeni ni marafiki walioanza shule pamoja. Tumaini ni mwenyeji wa mkoa wa Iringa na Mkakeni ni mwenyeji wa Kilimanjaro. Walipokuwa darasa la tatu, Mkakeni aliachwa yatima baada ya wazazi wake kufariki. Hali ya maisha ya Mkakeni ilianza kuwa duni. Mara nyingi alikosa huduma muhimu. Hatimaye Mkakeni alishindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa ada ya shule. Hali hii ilimhuzunisha sana Tumaini.

Hivyo, Tumaini akaamua kumwomba baba yake amlipie ada ya shule rafiki yake. Baba yake Tumaini alikubali kumsomesha Mkakeni hadi atakapomaliza elimu ya chuo kikuu.

**Maswali**

1. Tumaini na Mkakeni wana asili gani?
2. Unajifunza nini kutokana na habari hii?
3. Je, ni matendo gani mengine ya upendo na ushirikiano unayoyafahamu?

**Kazi ya kufanya**

Orodhesha watu wasio na asili ya Tanzania waishio Tanzania unaowafahamu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kujifunza mila na desturi mbalimbali

Ni vizuri kufahamu mila, desturi na asili ya watu mbalimbali unaoishi nao. Hivyo, unatakiwa kujifunza mila na desturi za watu wengine. Ukishazifahamu ni vyema uziheshimu na kuzijali. Ukifanya hivyo utaweza kujenga uhusiano mwema na kuishi kwa furaha katika jamii.

Soma ngonjera hii kwa sauti, kisha jibu maswali.

1. Hodi hodi twaingia
Kingindo, Kizaramo twakijua
Na nyinginezo twazichambua
Lugha zetu kuzitambua.

2. Mila na desturi zetu za asili
Tuzitunze kwa hali na mali
Tuziheshimu na kuzitii
Kuiendeleza yetu jamii.

3. Tuthamini tamaduni zetu
Tuachane na mbaya za wenzetu
Tusitiri vizuri miili yetu
Kwa mavazi yaliyo marefu.

4. Tujifunze mazuri ya wenzetu
Tusidharau na kuacha vya kwetu
Tuthamini ngoma za asili yetu
Mganda na Lizombe ndio zetu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Tule vyakula vyetu asili
Kuijenga yetu miili
Ugali, kande, matoke vyakula vyetu asili
Vya kisasa huathiri, tudumishe yetu asili.

**Kibwagizo**

Desturi twapigania
Wote twawakazania
Mila zetu za Tanzania
Tuzidumishe daima.

### Maswali

1. Unajifunza nini kutokana na ngonjera uliyoisoma?
2. Ni mambo gani ungependa kujifunza kuhusu makabila mengine?
3. Unafikiri mambo yote katika mila na desturi zetu ni mazuri?

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya kufanya

Chagua makabila matano (5) katika makabila ya Tanzania. Jaza chati ifuatayo inayoonesha asili ya watu mbalimbali. Namba moja imejazwa kama mfano.

| Na | Kabila | Mkoa | Chakula cha asili |
|---|---|---|---|
| 1 | Wamasai | Arusha /Manyara | Nyama na maziwa |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuheshimu utamaduni wa watu wengine

Ni vyema ukatambua kuwa tunaishi na watu wenye asili na tamaduni tofauti. Utagundua tofauti hizo katika mavazi, lugha, vyakula, ngoma, makazi na kazi wanazofanya.

Inakupasa kuheshimu mavazi, lugha, vyakula, ngoma na tamaduni za jamii zingine. Si vyema kuonesha dharau, kashfa au kauli mbaya juu ya mambo hayo.

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**



**B.**



**Kielelezo namba 3** Mavazi na ngoma ya asili yanayoonesha utamaduni wa watu mbalimbali.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Unaona nini katika picha hizi?
2. Je, mambo haya ni ya kawaida katika jamii yako?
3. Unajisikiaje unapocheza ngoma ya asili ya kabila tofauti na lako?
4. Utamsaidiaje mwenzako anayedharau mila za jamii zingine?
5. Ni matendo gani mengine utakayotenda kuheshimu utamaduni wa watu wengine?

**Kazi ya kufanya**

Orodhesha vifaa vinavyotumika wakati wa kucheza ngoma ya kabila mojawapo katika jamii yako.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kukemea mila na desturi potofu

Umejifunza kuwa ni muhimu kufuata mila na desturi za makabila yetu. Vilevile, inakupasa utambue kuwa kuna mila na desturi ambazo sio nzuri kuzifuata.

Soma habari hii, kisha jibu maswali.

Losinyari na Esupati ni watoto wa Mzee Lendise. Losinyari ana umri wa miaka kumi wakati Esupati ana miaka tisa. Losinyari ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Miti Mirefu. Esupati hajaandikishwa shule, hivyo hubaki nyumbani akifanya kazi na mama yake. Losinyari alimuuliza baba yake sababu za dada yake kutokwenda shule. Mzee Lendise alimjibu kuwa mila za jamii yao haziruhusu msichana kwenda shule. Losinyari alijaribu

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kumshauri baba yake ampeleke Esupati shule lakini ilishindikana. Esupati alikuwa analia kila alipowaona watoto wenzie wakienda shule. Losinyari baada ya kuona juhudi zake zimeshindikana aliamua kwenda kumwambia mwalimu mkuu. Mwalimu mkuu alimuita Mzee Lendise ili atoe sababu ya Esupati kutoandikishwa shule. Mzee Lendise alisema "Mila na desturi za jamii yetu zinakataza kumsomesha msichana." Mwalimu mkuu alisema "ni haki ya mtoto kupata elimu, msichana au mvulana. Nakuagiza kesho asubuhi umlete Esupati shuleni. Ukishindwa kumleta, utachukuliwa hatua za kisheria." Siku iliyofuata Esupati aliandikishwa shule. Losinyari alifurahi sana dada yake kuanza shule.

**Maswali**

1. Unajifunza nini kutokana na kisa hiki?
2. Je, mambo kama haya yapo katika jamii yako?
3. Utafanya nini iwapo jambo kama hili litatokea katika familia yako?
4. Ni desturi gani potofu zinazofanywa katika jamii yako?

**Kazi ya kufanya**

Jadili na mzazi au mlezi kuhusu mila na desturi potofu za makabila mbalimbali. Andika maelezo kwenye karatasi.

## Kujenga urafiki unaofaa

Urafiki ni uhusiano unaofaa kati ya mtu mmoja na mwingine. Zipo njia nyingi za kujenga urafiki. Njia hizo ni pamoja na kusaidiana katika mambo mbalimbali na kucheza pamoja. Njia nyingine ni kusoma na kufanya kazi pamoja.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tazama picha hizi, kisha jibu maswali.

**A.**



**B.**



**C.**



**Kielelezo namba 4** Kujenga urafiki unaofaa

**Maswali**

1. Je, picha A, B na C zinaonesha matendo gani?
2. Je, matendo gani mengine yanajenga urafiki unaofaa na watu wengine?
3. Ni matendo gani unayopenda kutendewa na rafiki yako?
4. Ni matendo gani utakayotenda kujenga urafiki na mwenzako?
5. Kuna umuhimu gani wa kuwa na rafiki?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Chunguza marafiki zako kisha andika matendo yanayofaa kuigwa kutoka kwao.

## Kutofautisha rafiki anayefaa na asiyefaa

Kuwa na marafiki ni jambo zuri. Tunahitaji kuwa na rafiki anayefaa ili kuishi kwa furaha na mafanikio. Hivyo inakupasa utambue sifa za rafiki anayefaa na asiyefaa.

Soma kisa hiki, kisha jibu maswali.

Leila ni mwanafunzi wa darasa la tatu. Yeye huonesha tabia inayofaa shuleni na nyumbani. Wanafunzi wengi darasani kwao walimpenda na kuomba kujenga urafiki naye. Julipendo na Beda walikuwa miongoni mwao. Siku moja Leila alikubali kwenda nyumbani kwa akina Julipendo wakasome pamoja. Alipofika akaambiwa Julipendo hayupo na wazazi wake hawakujua alipokwenda. Leila alimshangaa rafiki yake kwa kumdanganya.

Siku nyingine Julipendo alimshawishi Leila watoroke shule waende wakaangue maembe. Leila alikumbuka alivyodanganywa hivyo alikataa. Ilipofika jioni ya siku hiyo, Leila alishikwa na ugonjwa wa malaria. Beda alimtembelea Leila baada ya kutomwona shuleni. Siku iliyofuata akatoa taarifa kwa mwalimu wa darasa kuhusu ugonjwa wa Leila. Pamoja na Julipendo kupata taarifa za ugonjwa hakwenda kumpa pole Leila.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Maswali

1. Unajifunza nini kutokana na kisa ulichosoma?
2. Je, tabia kama hizi zipo miongoni mwa wanafunzi wenzako?
3. Ni rafiki yupi anayefaa kati ya Beda na Julipendo?
4. Kuna faida gani za kuwa na rafiki anayefaa katika maisha yetu?

### Kazi ya kufanya

Andika habari fupi kwenye daftari lako kuhusu rafiki yako. Eleza sababu za kumchagua kuwa rafiki yako.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi

1. Taja mambo yanayotambulisha utamaduni wa kabila lako.
2. Eleza unavyojisikia unapotendewa matendo mema na watu wenye asili tofauti.
3. Eleza sifa za rafiki anayefaa.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kutambua nchi marafiki wa Tanzania**

Nchi marafiki ni nchi zenye ushirikiano na uhusiano mzuri katika mambo mbalimbali.

Soma mazungumzo kati ya Neema na Musa, kisha jibu maswali.

**Neema** Habari Musa.

**Musa** Nzuri Neema.

**Neema** Mimi ni mwanafunzi wa darasa la tatu. Je, wewe unasoma darasa la ngapi?

**Musa** Mimi nasoma darasa la tano.

**Neema** Nina maswali yananitatiza. Je, naweza kuuliza?

**Musa** Ndiyo, uliza.

**Neema** Nchi zipi ni marafiki wa Tanzania?

**Musa** Swali zuri. Nchi marafiki wa Tanzania ni kama vile Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda.

**Neema** Ahaa kumbe! Hizo ndizo nchi marafiki wa Tanzania. Je, kuna nchi nyingine tofauti na hizo?

**Musa** Ndiyo, zipo nchi nyingine zaidi ya hizo. Mfano, Malawi, Zambia, Msumbiji na nyingine nyingi.

**Neema** Je, kuna faida yoyote ya kuwa na urafiki na nchi hizo?

**Musa** Ndiyo.

**Neema** Ahaa! Faida hizo ni zipi?

**Musa** Raia wa nchi hizo huwa huru kufanya biashara na kupata pesa. Pia, watu hujenga urafiki wa kutembeleana.

**Neema** Nashukuru sana rafiki yangu kwa majibu mazuri.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Musa** Nashukuru pia. Utakapokuwa na maswali mengine uje uniulize.

**Neema** Kwa heri, Musa.

**Musa** Wasalimie nyumbani.

## Maswali

1. Taja nchi marafiki wa Tanzania unazozifahamu
   (a) ________
   (b) ________
   (c) ________

2. Kuna faida yoyote ya kuwa na urafiki na nchi nyingine? Taja sababu mbili za jibu lako.
   (a) ________
   (b) ________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Asili** | mwanzo wa mtu au kitu |
| **Desturi** | jambo la kawaida linalotendwa kila siku |
| **Mila** | mambo ya asili yanayofanywa na jamii kwa muda mrefu |
| **Utamaduni** | mila, asili na desturi za jamii fulani |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Jaribio la Kwanza

## Sehemu A

**Chagua herufi ya jibu sahihi kwa kuandika herufi hiyo katika kisanduku.**

1. Faida mojawapo ya kuwashirikisha watoto katika kufanya maamuzi ni
   a. kuleta upendo na umoja
   b. kuleta upendeleo
   c. kuleta ugomvi

2. Nyama na maziwa ni chakula cha asili cha jamii ya kabila la
   a. Wazaramo
   b. Wasukuma
   c. Wamasai

3. Wimbo wa taifa unapoimbwa shuleni tunatakiwa
   a. tukae chini
   b. tutulie na kusimama wima
   c. tukimbie haraka mstarini

4. Moja kati ya hizi si alama ya Taifa letu, nayo ni
   a. fedha zetu
   b. polisi
   c. mwenge wa uhuru

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sehemu B

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika jibu sahihi.**

5. Bendera ya Tanzania ina rangi ____________.
6. Jina Tanzania ni muungano wa majina Tanganyika na _________.
7. Shule ni sehemu ya jamii inayowapatia watoto _______ na _______ bora.
8. _______ na Julius Nyerere walikuwa waasisi wa nchi yetu.
9. _______ hutokana na vyanzo mbalimbali kama mvua, mito, chemchemi, bahari na maziwa.

## Sehemu C

**Oanisha fungu (A) na (B) ili kuleta maana iliyo sahihi. Weka jibu kwenye kisanduku.**

| Fungu (A) | | Fungu (B) |
|---|---|---|
| 10. Kujisomea | ☐ | A. vitu vinavyoweza kuleta maendeleo. |
| 11. Kutunza mazingira | ☐ | B. ni muhimu kwa maisha ya watu, mimea na wanyama. |
| 12. Maji | ☐ | C. ni sehemu ya matendo yanayoonesha nidhamu binafsi. |
| 13. Rasilimali | ☐ | D. ni kuyalinda na kuyahudumia ili yavutie. |
| 14. Uadilifu | ☐ | E. ni kuishi kwa kufuata maadili ya jamii. |
| | | F. ni muhimu kwa maisha ya mimea. |
| | | G. kutii kila kitu. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sehemu D

**Jibu ndiyo kwenye sentensi ya kweli na hapana kwenye sentensi isiyo kweli.**

15. Ulemavu ni hali ya kuwa na kasoro ya kimaumbile ________________
16. Wimbo wa Tanzania, Tanzania una beti mbili_________
17. Watu wanaowajibika kutunza rasilimali za shule ni walemavu tu________________
18. Kwa kutumia lugha inayofaa kuwasiliana na mwenzako utaepuka ugomvi_____________
19. Moja ya haki ya watoto ni kupata elimu bora_________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Jaribio la pili

### Sehemu A

**Chagua herufi ya jibu sahihi kwa kuandika herufi yake kwenye kisanduku.**

1. Moja ya nchi zifuatazo si rafiki wa Tanzania.
    (a) Afrika
    (b) Kenya
    (c) Uganda

2. Vitu vinavyotambulisha Taifa ni
    (a) alama za miti
    (b) alama za Taifa
    (c) maji

3. Matendo yanayojumuisha kuipenda na kujivunia shule ni
    (a) kutunza mazingira ya shule
    (b) kutoroka shuleni
    (c) kupigana shuleni

4. ______ ni uwezo alionao mtu ambao humwezesha kufanya jambo fulani.
    (a) Kipaji
    (b) Utamaduni
    (c) Mwenge

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sehemu B

Linganisha kifungu cha maneno kutoka **kundi (A)** na kifungu cha maneno kutoka **kundi (B)**. Kisha andika herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku ili kuleta maana.

| Kundi ( A ) | | Kundi ( B ) |
|---|---|---|
| **Mfano** Kabila la Kinyamwezi | C | A. kutupa vitu vyenye sumu |
| 5. Vivutio vilivyopo Tanzania | | B. kufichua uovu |
| 6. Moja ya haki za watoto | | C. mkoani Tabora |
| 7. Uchafuzi wa vyanzo vya maji | | D. kupata elimu bora |
| 8. Matendo ya uaminifu | | E. mbuga za wanyama |
| 9. Vifaa vinavyotumika kuchezea ngoma | | F. kibwaya na njuga |

## Sehemu C

**Andika ndiyo kwa sentensi iliyo sahihi na hapana kwa sentensi isiyo sahihi.**

10. Miongoni mwa nchi marafiki wa Tanzania ni Kenya na Uganda.
11. Chemchemi ni maji yanayotoka ardhini.
12. Ugomvi, kutoaminika na kukosa amani ni mambo ya msingi katika maisha.
13. Kusoma kwa bidii, kuwapenda wengine na kutii wazazi ni wajibu wa watoto.
14. Vyanzo vya maji ni mawe, mchanga na nyasi.
15. Wimbo wa Taifa una beti nne.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sehemu D

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika jibu sahihi.**

16. Amani, upendo, umoja, uzalendo, mshikamano na utu ni ________ za Taifa.

17. Kivutio kimojawapo cha watu nchini Tanzania ni ________

18. Taja alama tano (5) zinazoonekana kwenye nembo ya Taifa.

    a. ________

    b. ________

    c. ________

    d. ________

    e. ________

19. Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanzania alikuwa ________ .

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



# 1. Tanzania Tanzania, nakupenda kwa moyo wote




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## 2. Wimbo wa Taifa




FOR ONLINE USE ONLY

Vitabu vingine kutoka

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## Darasa la Tatu



















Uraia na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu

ISBN 978-9987-09-315-1

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*